# MUWALA KATIKA VIKATUNI VYA *SHUJAAZ*: MTAZAMO WA KIUCHANGANUZI MAKINIFU WA DISKOSI

***Dimbu, S.L. and Kobia, J. M.***
*Chuo Kikuu cha Chuka, S.L.P. 109-60400, Kenya Barua Pepe: dimbuliana@gmail.com, jkobia2001@yahoo.com; jkobia@chuka.ac.ke*

**How to cite:**
J.M Kobia, S.L Dimbu muwala katika vikatuni vya *shujaaz*: mtazamo wa kiuchanganuzi makinifu wadiskosi. Isutsa, D.K. (Ed) *Proceedings of the 8th International Research Conference held in Chuka University from 7th to 8th October 2021, Chuka, Kenya, p.242-251*

**IKISIRI**
Vikatuni vina wajibu muhimu katika aushi ya watoto na vijana ulimwenguni. Huenda ndio sababu Karne ya 21 imeshuhudia ongezeko la tafiti kuhusu vikatuni. Kumekuwepo na tafiti nyingi kuhusu muwala katika uwanja wa kiusomi. Tafiti za awali zilijikita katika muwala kwenye makala, magazeti, tasnifu, vitabu na vikatuni. Hata hivyo, hakuna utafiti kuhusu muwala katika vikatuni wa *Shujaaz*. Makala hii ililenga kuziba pengo hili. Utafiti huu ni kueleza namna muwala ulivyokuzwa katika diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*. Diskosi hii ni jarida linalowasilishwa kupitia msimbo wa Sheng ambalo hulenga vijana kuanzia umri wa miaka 12 hadi 35. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi. Mojawapo wa madhumuni ya nadharia hii ni kusaidia katika uchanganuzi wa diskosi ili kufichua imani za kiitikadi zinazochukuliwa kuwa za ukweli na kukubaliwa katika jamii. Data ya makala hii ilitokana na sampuli ya nakala 35 zilizoteuliwa kimakusudi kwa kuzingatia kigezo cha yaliyomo. Mpango wa kimaelezo ulitumika kuchanganua na kuwasilisha matokeo. Muwala hukuzwa kupitia: mada, sauti za kionomatopeya, maandishi panelini, maelezo ya mwandishi na uzungumzi nafsi. Aina ya muwala uliokuzwa ulitokana na msuko wa hadithi, muwala wa jumla na mada. Matokeo ni muhimu katika kuangazia namna kampuni ya *WellTold Story* ilivyotumia maarifa ya kiusuli katika jamii kukuza muwala wa jumla kama mkakati wa kuendeleza na kuwawekea vijana vizingiti ili kuwadhibiti.
**Istilahi Muhimu:** Paneli, Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi, Mchakato wa Kijamii, Diskosi na Vijana

## UTANGULIZI

Muwala ni sifa ya kimsingi ya diskosi (Wang & Guo, 2012). Muwala huchangia katika uwasilishaji wa vikatuni vya *Shujaaz* kwa njia mbalimbali: humfaa msomaji kuelewa na kufahamishwa. Muwala hutoa mwelekeo kwa msomaji kuelewa kwa ufasaha. Kwa misingi hii muwala unapaswa kutafitiwa kwa undani zaidi. Dhana hii hurejelea mfuatano wa matukio kwa utaratibu kiasi kwamba yanakuwa na mshikamano wa mawazo katika diskosi nzima (Nangira, 2004). Aidha, muwala huangazia mshikamano na uhusiano wa dhana katika usemi. Hii ina maana kuwa muwala humwelekeza msomaji kuunganisha paneli moja na nyingine au wazo na wazo jingine. Muwala humfaa mwandishi na msomaji kutathmini mwingiliano na msuko wa hadithi katika vikatuni.

Diskosi ni dhana pana na ina fasiri nyingi kulingana na mitazamo ya kiisimu, kisosholojia na kifilosofia. Kiisimu, diskosi inafafauliwa kuwa jumla ya shughuli za mawasiliano zinazojumuisha usemi, muktadha na sheria za kufasiri ujumbe (Taylor, 2001). Kwa mujibu wa Bhatia (2013) uchanganuzi makinifu wa diskosi ni ufichuzi wa itikadi na miundo fiche ya mamlaka kwenye mifumo ya kijamii, kisiasa na kitamaduni kupitia lugha. Matumizi mabaya ya mamlaka, hegemoni na ukosefu wa usawa hudhihirika kupitia kwa mitagusano ya jamii na hufichama kwenye lugha ya kuvutia na matumizi ya msamiati wa adabu. Diskosi ya *Shujaaz* haitumiki katika ombwe tupu bali hutekeleza wajibu wa kipekee katika miktadha mbalimbali ya maisha ya vijana. Miktadha hii ni pamoja na: kisiasa, kitamaduni, kisaikolojia na kiuchumi. Kulingana na Fairclough & Wodak (1997) diskosi haizalishwi wala haiwezi kueleweka bila uzingatifu wa muktadha mahususi wa matumizi. Diskosi hii ni zao la michakato mbalimbali ya kijamii wanamoishi vijana (Kale, 2003).

Lugha ya ishara, michoro ya picha na istilahi zilizoandikwa hurejelewa kama dhana moja (Eisner, 1985). Wazo hili la Eisner (ametajwa) linashadidiwa na Neil (2012) anaposema kuwa michoro ya picha za michoro si utanzu wa sanaa bali ni lugha inayokua. Dhana ya vikatuni inafafanuliwa na McCloud (1993) kuwa ni michoro ya picha iliyopangwa pamoja katika msuko ili kupitisha maarifa au kuzua ujumi. Ifahamike kuwa, fasiri ya McCloud

(ametajwa), haijakamilika kwani inatenga kazi zinazowasilishwa kwa michoro ya picha iliyoambatanishwa na maandishi (Neil, 2005). Mfano wa kazi ambazo michoro ya picha huambatanishwa na maandishi ni diskosi ya *Shujaaz*. Isitoshe, fasiri ya McCloud (ametajwa) ilipuuza kazi inayowasilishwa kwa paneli moja na kuviondoa katika ulimwengu wa vikatuni (Jacobs, 2007). Ikumbukwe kuwa vikatuni ni kifaa cha jamii ambacho ni zao la shughuli mbili za binadamu: uchoraji na uandishi. Msuko uliokuzwa na michoro ya picha katika data ya makala hii zilisheheni "lugha ya kutazamwa". Lugha hii ni zao la uandishi na uchoraji wa michoro ya picha ili kuwasilisha kazi ya vikatuni ambayo ilitafitiwa kiisimu (Neil, 2012).

**MWAUO WA MWANDISHI**

Diskosi husheheni maarifa na kumbukumbu za michakato ya kijamii (Van Dijk, 1998). Wakati wa vita, mipaka ya kejeli huwa baina ya "sisi" dhidi ya "wao". Vikatuni huwa havikuzi tu mgawanyiko wa kisiasa bali huwa kitambulisho cha taifa (Streicher, 1967). Scott (2011), alitafiti kuhusu vikatuni na ukosefu wa amani. Alifafanua maudhui ya vita na uzalendo katika historia ya utamaduni wa nchi ya Marekani kuanzia Vita vya Pili vya Dunia hadi vita vya uvamizi wa Taifa la Iraq. Alibainisha dhima ya vikatuni kuwa ya kuburudisha na kufahamisha katika kipindi cha vita. Viliburudisha nyakati za huzuni, kupigania amani na demokrasia. Utafiti wa Scott (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuchanganua diskosi ya *Shujaaz* katika kipindi maalumu cha kihistoria ambacho kilikuza muwala wa jumla. Tofauti ni kuwa utafiti wa Scott (2011), ulihusisha sampuli ya vikatuni vilivyochapishwa nchini Marekani ilhali sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kutoka vikatuni vinavyochapishwa nchini kenya.

Uchanganuzi makinifu wa diskosi hufafanua diskosi kama mchakato wa kijamii na huangazia diskosi katika kujikita kwa vipashio vya kiisimu na diskosi kama mazoea ya kijamii (Faircough, 1992). Matara (2014), alitafiti kuhusu uchanganuzi wa lugha ya amani na maridhiano katika muziki nchini Kenya (2008-2012). Utafiti wake msisitizo uliwekwa kwenye vipashio vya kiisimu pamoja na uchanganuzi wa diskosi kama mchakato wa kijamii. Utafiti wa Matara (2014), ulifaa utafiti huu katika kuchanganua baadhi ya data ya utafiti huu ambayo iliwasilishwa kwa msimbo wa Sheng. Sawia na utafiti wake utafiti huu ulitumia nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi. Tofauti ni kuwa utafiti wa Matara (2014), ulihusu sampuli ya nyimbo ilhali sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kutokana na vikatuni. Aidha, diskosi huundwa na jamii, matumizi ya lugha huamuliwa kijamii na lugha hubadilika kulingana na hali ya jamii (Fairclough, 2006). Belhassena (2014), alitafiti kuhusu vipengele vya mtagusano wa lugha mbalimbali katika vikatuni vya Taifa la Algeria katika *Sabaous Houna Fighter*. Anasema kuwa kuwasilishwa kwa vikatuni hivi katika msimbo ulitegemea: shinikizo la kijamii, chombo cha kuangazia masuala ya kijamii na kusambaza kaida za kijamii. Utafiti wa Belhassena (ametajwa), ulifaa utafiti huu katika kuangazia matumizi ya msimbo wa Sheng miongoni mwa vijana kuwa mchakato wa kijamii. Kupitia kwa msimbo huu *Shujaaz* hutekeleza wajibu wa kuelimisha na kuburudisha. Tofauti ni kuwa utafiti wa Belhassena (2014), ulihusu sampuli kutoka vikatuni vya *Sabaous Houna Fighter* ilhali sampuli ya utafiti iliteuliwa kutoka jarida la *Shujaaz*.

**MISINGI YA NADHARIA**

Makala hii iliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi ambayo hudokeza kuwa diskosi na jamii hutegemeana na kujengana. Waasisi wa nadharia hii ni pamoja na Fairclough & Wodak (1997. Nadharia hii hutoa sababu zinazofanya diskosi ambazo ni zao la jamii kukubaliwa jinsi zilivyo (Fairclough, 1995). Fairclough (1992), anasema kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi unaweza kutokea kwa namna tatu. Kwanza, uchanganuzi makinifu wa diskosi hujikita katika vipashio vya kiisimu kama vile leksimu, sarufi, muwala na muundo wa diskosi. Mtazamo huu ulifaa makala hii katika kuchanganua namna muwala ulivyopatikana katika vikatuni vya *Shujaaz*. Pili, uchanganuzi unashughulikia diskosi kama mchakato wa kijamii. Hii ina maana kuwa diskosi ni mali ya jamii na hutekeleza wajibu wake kutegemea matarajio ya wanajamii ambamo diskosi hiyo imezalishwa. Matarajio haya huwa sehemu muhimu ya maarifa ya kiusuli yanayokuza muwala wa kijumla. Hatimaye, diskosi ya *Shujaaz* ilishughulikiwa kama suala la mazoea ya kijamii. Mtazamo huu ulifafanua kuwa diskosi huzaliwa, husambazwa, huenezwa na kutumiwa katika jamii. Mikakati mbalimbali ya mazoea ya kijamii hutumiwa kuipa diskosi hii utambulisho katika mazingira ilimosomwa na hivyo kukuza muwala wa kijumla. Mihimili iliyoongoza makala hii ni pamoja na: Diskosi huundwa na jamii. Matumizi ya lugha huamuliwa kijamii na lugha hubadilika kulingana na hali ya jamii, Diskosi husaidia katika kuunda na kubadilisha maarifa, mahusiano ya jamii na utambulisho wa jamii, Diskosi huundwa na mahusiano ya uwezo na husheheni itikadi. Mhimili huu hudokeza athari za kijamii katika diskosi, diskosi huundwa na mahusiano ya uwezo na husheheni itikadi na diskosi huundwa na mahusiano ya uwezo na husheheni itikadi.

**MBINU YA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia mpango wa kimaelezo katika kuchanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Usampulishaji katika makala hii ulikuwa mchakato wa kuteua kundi ndogo kutoka katika kundi kubwa la nakala za *Shujaaz* zilizotafitiwa ili kuafikia malengo ya utafiti (Kothari, 2009). Kwa mujibu wa Gay (1992) mtafiti huteua sampuli kwa sababu ya kuwepo kwa ufinyu au udhaifu fulani ambao huzuia kutafitia idadi lengwa yote. Ufinyu na udhaifu uliomkumba mtafiti unafafanuliwa na Mugenda na Mugenda (1999) wanaposema kuwa rasilimali na wakati ndivyo vizuizi vikubwa katika kufanya maamuzi kuhusiana na uteuzi wa sampuli. Mtafiti aliteua kimakusudi jumla ya nakala 35 kwa kuzingatia kigezo cha yaliyomo. Mugenda na Mugenda (1999) wanasema kuwa katika mbinu ya kimakusudi, mtafiti huwa na uhuru wa kuteua sampuli zilizo na data iliyohitajika. Mtafiti aliteua nakala moja kwa kila matoleo matatu, kuanzia toleo la kwanza Februari mwaka wa 2010 hadi toleo la Disemba mwaka wa 2018.

Kiwango cha sampuli iliyoteuliwa kilikuwa takribani asilimia thelathini na tatu nukta tatu ya jumla ya nakala zilizochapishwa katika kipindi hiki. Asilimia ambayo iliafikiana na mawazo ya Mulusa (1990) anapopendekeza kuwa thuluthi ya idadi lengwa inatosha kutumiwa katika kufanya makadirio ya sifa zinazochunguzwa katika utafiti.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Vipengele vifuatavyo hukuza muwala katika diskosi ya vikatuni vya *Shujaaz*:

### Mada na Muwala

Mada ni mapatano baina ya washiriki katika mawasiliano kulingana na mhimili wa umuhimu. Uteuzi wa mada ya diskosi hutegemea kilicho muhimu hapa, kwangu na kwake katika kipindi fulani (Coulthard, 1981). Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa kuna nakala ya #29 yenye hadithi ya mada: "Mtiche Akikosa, Utagwara". Maswali yaliyoongoza uelewaji wa hadithi hii ni pamoja na: Kwanza, namna mada ilivyochangia uelewaji wa hadithi? Pili, namna mada ilivyokuza muwala? Hatimaye, namna mada ilivyokuza muwala uliotokana na msuko na muwala wa kijumla? Muwala wa kijumla ulikuzwa na maarifa ya kiusuli ya hadhira lengwa kuhusu matukio mbalimbali hadithini (Habwe, 1999). Muwala ulikuzwa na mada kwa kueleza ni kwa nini paneli zilihusiana kimaana katika kujenga msuko wa hadithi (Brown & Yule, 1983). Tazama:

*Mtiche akikosa? Utagwara!!*
Mwalimu akikosa? Utafeli!!
(*Shujaaz*Chapta #29, ukurasa wa 19)

Muwala wa kijumla ulikuzwa na mada hii ikizingatiwa kuwa baadhi ya hadhira lengwa ni wanagenzi au waliwahi kuwa. Huenda wameshuhudia visa vya walimu kutohudhuria vipindi vya masomo shuleni. Paneli ya kwanza ilisimulia shughuli walizoshiriki wanafunzi wakati kipindi cha masomo walimu waliposa kuhudhuria. Matukio yafuatayo yalibainika:

(*Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 19




Utangulizi wa hadithi ni mandhari ya darasani. Wanafunzi walishiriki katika kuchongoana, kulala kwenye dawati, kusimama darasani na kupiga gumzo. Hizi ni athari za walimu kutohudhuria vipindi vya masomo shuleni. Paneli ya mwisho isiyokuwa na uhusiano wa ujirani na paneli ya kwanza matukio yafuatayo yalidhihirika:

(*Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 23)

Muktadha wa mandhari ni ukumbi wa shule kulikofanyika mkutano wa wazazi na walimu. Wazaziwalitaja sababu za walimu kukosa kuhudhuria vipindi vya masomo kuwa:

*Mwalimu mwingine anasafirisha bodaboda mchana.*




Mwalimu mwengine ni mhudumu wa bodaboda mchana (wakati ambao anapaswa kuwa shuleni).

*Performance imeharibika juu walimu wako biashara mchana.*
Matokeo (ya mtihani) yamedorora kwa sababu ya walimu kufanya biashara mchana (wakati ambao wanapaswa kuwa shuleni).
*Nilienda M-Pesa mchana mwalimu wa class 3 akaniitisha pesa za hio tuition*.
Nilienda kutafuta huduma za *M-pesa* mchana (wakati ambao mwalimu anapaswa kuwa shuleni akifunza) mwalimu wa darasa la tatu akaniagiza pesa za masomo ya ziada.
*Ndio! Hata mimi ninaunga mkono hio proposal.*
Naam, hata nami ninaunga mkono pendekezo hilo (kupewa uhamisho kwa naibu wa mwalimu mkuu).

Kauli hizi ni maoni ya wazazi kuhusu vichocheo vya walimu kutohudhuria vipindi vya masomo. Kwanza, kuna mwalimu ambaye ni mhudumu wa bodaboda badala ya kuwa kazini. Pili, kiwango cha masomo kilididimia kwa sababu ya walimu kushiriki biashara wakati waliopaswa kuwa shuleni. Tatu, walimu wanarandaranda njiani wakiwaitisha wazazi pesa za mafunzo ya ziada. Hatimaye, mmoja wao aliunga mkono pendekezo la naibu wa mwalimu mkuu kupewa uhamisho. Dhana ya mada baina ya paneli ya kwanza na ya mwisho ilifasiriwakwa kuzingatia uhusiano wa matukiobaina ya paneli hizi mbili. Ingawa, hazipo katika mahusiano ya ujirani. Yaliyomo yalihusu mada ya hadithi. Paneli ya kwanza ilitoa athari na ya mwisho ilitoa kiini cha walimu kutohudhuria vipindi vya masomo. Paneli hizi zilihusiana kwa njia spesheli. Kilichoziweka pamojani suala la walimu kukosa kuhudhuria vipindi vya masomo shuleni. Suala lilosababisha kufeli kwa wanafunzi. Kwa mujibu wa Danes (1974), muwala wa diskosi huathiriwa na mshikamano na mwingiliano wa maudhui yanayochangia kukuza mada kuu. Muwala ulikuzwa na matukio panelini kuwa na uhusiano wa dhana. Dhana hizi zilikuwa na ukweli fulani wa mahusiano ya kimaana na mada kuu ya hadithi (Van Dijk, 1987). Mahusiano ya mada yalikuwa kiini cha paneli hizi kusomeka kama sehemu ya hadithi iliyokuwa ikisimuliwa.

Masuala yafuatayo ni baadhi ya elementi zilizokuza muwala baina yapaneli ya kwanza na ya mwisho:


i. Hadithi hii iliwasilishwa kupitiadiskosi ya*Shujaaz* ambavyo huchapishwa nchini Kenya. Hivyo, matukio katika paneli ya kwanza na paneli ya mwisho yalihusiana moja kwa moja na muktadha wa wanamoishi vijana. Muwala wa jumla uliokuzwa ulitokana na maarifa ya kiusuli walionayo vijana kuhusu athari na sababu za walimu kutohudhuria vipindi vya masomo shuleni.
ii. Wahusika vibonzo kwenye paneli hizi walitumia msimbo wa Sheng ambao ulihusishwa na vijana. Vijana walijitambulisha na wahusika wanafunzi katika paneli ya kwanza na kuwaona kama wenzao.
iii. Wahusika katika paneli hizi ni wazazi, wanafunzi na walimu ambao ni washika dau katika sekta ya elimu.
iv. Suala muhimu ni kumulika walimu wasiowajibika kwa kukosa kuhudhuria vipindi vya masomo shuleni.
v. Muktadha wa mandhari ya paneli hizi ni shuleni: Paneli ya kwanzani darasani na paneli ya mwisho ni katikaukumbi wa mikutano ambao ulihusiana moja kwa moja na mada iliyohusu walimu kutohudhuria vipindi vya masomo shuleni.
vi. Elementi nyingine ni kama vile sentensi, nomino na vishazi ambavyo vilihusiana kimaana na madakatika paneli ya kwanza na paneli ya mwisho. (Habwe, 1999: 186)



Ingawa, paneli ya kwanza na paneli ya mwisho zilisambazwa katika sehemu tofauti za hadithi. Muwala ulichangiwa na elementi zilizounda mshikamano wa mawazo au dhana baina ya paneli hizi. Mwandishi alihakikisha kuwa chochote alichoangazia kilitimiza kigezo cha umuhimu (Coulthard, 1981), ili paneli zitimize mahitaji ya muktadha wa kiisimu na kimandhari. Muwala baina ya paneli hizi ulibainika nje ya mipaka ya mfuatano ya namna paneli zilivyofuatana katika hadithi iliyosimuliwa. Ishara panelini zimejengeka kwenye misingi ya kufasiriwa na msomaji kwa kuzingatia uhusiano wa dhana moja na nyingine. Licha ya ukweli kuwa hazipo katika mahusiano ya ujirani. Anavyosema Groensteen (1999), ni kuwa paneli hutagusana kimaana bali si lazima ziwe katika ujirani ila ni paneli zote hadithini. Paneli moja huhusiana na nyingine kwa sababu kila paneli huwepo katika vikatuni kwa kuhusiana na nyingine (Groesteen, 2007). Hata hivyo, baadhi ya paneli hazina uhusiano wa moja kwa moja na mada. Ukosefu wa mshikamano wa kimaana baina ya paneli ulisambaratisha mfumo wa ukuzaji wa mada kuu ya hadithi (Fries, 1983 katika Wang & Guo, 2014).

Tazama mfano: (*Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 21)
Yanayotendeka panelini hayana uhusiano wa moja kwa moja na mada kuu ya hadithi:

Mwalimu: *Unajua wewe ni mrembo hadi other women wameogopa kuingia hoteli?*
Unajua wewe ni mrembo hadi wanawake wengine wameogopa kuingia mkahawani?
Mama yake Malkia: *Stop it with the flattery.*
Wacha kunihadaa.




Mazungumzo panelini hayaambatani na mahitaji ya mada ya hadithi. Yanalazimu swali, "Je, ni kwa nini yawepo hadithini na kwa muktadha upi?" Mkondo wa mazungumzo baina ya wahusika panelini haukuzi muwala ulioletwa na msuko wa matuio hadithini. Kimaana paneli hii iko nje ya mada. Iliangazia masuala ambayo yakitathminiwa kivyake hayakuwa na uhusiano wa moja kwa mojana mada kuu. Mazungumzo baina ya mwalimu na Mama yake Malkia yalikuza muwala wa kijumla. Yalihitaji maarifa ya kiusuli kutokakatika nakala tofauti. Katika nakala ya #100, Malkia anasema:

(*Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 16)

*…My mum huwa busy kila times so mara most yeye hunipeleka kwa my nyanya my dada hu-work Saudi Arabia. Anatumanga dooh ya fees lakini huwa hakuji home…*

…Mama yangu huwa na shughuli nyingi ila wakati aghalabu hunipeleka kwa nyanya yangu. Baba yangu hufanya kazi katika nchi ya Saudi Arabia...

Kauli hii iliibua dhana kuwa Mama wa Malkia ni mzazi mtepetevu. Alipuuza kuzungumza na Malkia kuhusu masuala yaliyomhusu kama kijana msichana. Anaenda kukutana mikahawani na mwalimu aliyedhani angemchumbia. Huenda, ni kwa sababu mumewe hufanya kazi nchiniSaudi Arabia na haji nyumbani (Tazama: *Shujaaz* chapta #100, ukurasa wa 16). Kwa mujibu wa Van Dijk (2001), nguvu za kushawishi huwekewa msingi na maarifa, habari na mamlaka. Mwalimu alitumia uwezo wa kuwa mwalimu kumshawishi Mama yake Malkia kumlipia Malkia masomo ya ziada.

**Sauti za Kionomatopeya**

Sauti ya kionomatopeya ni neno linaloiga sauti ya kitu fulani (Dofs, 2008). Huwasilisha sauti ya kitu, kiumbe au hali. Sauti hii huiga au huzalisha au huwakilisha sauti ya kimsingi ya kitu Fulani. Kuwepo kwa sauti za kionomatopeya vikatuni ni hustawisha maana ya picha za michoro "zilizonyama" (McCloud, 1993). Anavyosema Beck (1999), ni kuwa sauti za kionomatopeya si sehemu ya maneno ya mwandishi wala michoro ya picha na hupewa nafasi ndogo panelini. Huungana na michoro ya picha ili kuwasilisha maana yasiyowasilishwa kwa maneno au michoro ya picha pekee (Harvey, 2001). Tazama mfano, sauti ya kionomatopeya, "KUKURIKOO!!!"

(*Shujaaz* chapta #61, ukurasa wa 30)




*Kukurikoo!!!* ni sauti iliyoiga sauti ya jogoo anapowika. Iliashiria kupambazuka, yaani wakati wa majogoo; kumekucha. Ufasiri huu ulitokana na maarifa ya kiusuli ya msomaji kuwa, kuwika kwa jogoo uliashiria mapambazuko. Brown na Yule (1983), wanasisitiza kuzingatiwa kwa maarifa ya kiusuli katika kufasiri muwala. Panelini sauti hii iliambatana na picha za michoro ya miale ya jua angani. Ilitoka kwa nyumba, alikolala jogoo. Kwa mujibu wa Petersen (2007), kuna uhusiano wa kimaana baina ya sauti ya kionomatopeya na michoro ya picha. Michoro hii hutoa maelezo zaidi katika kujenga maana ya panelini. Sauti hizi zinapochanganuliwa picha za michoro huzingatiwa. Sauti *kukurikoo!!!* iliyaweka matukio panelini na zilizofuatia kwenye kipindi maalumu cha kiwakati. Matukio yalitokea "wakati wa majogoo", yaani alfajiri na mapema. Maana iliyopatikana ni "siku iliyofuata asubuhi na mapema." Mhusika Malkia, Kazuri na Jipendo katika paneli zilizotangulia walihudhuria "Disko Matanga" usiku. Hata hivyo, Malkia alikosa kurudi nyumbani pamoja nao. Paneli iliyofuata mhusika Malkia aliamka asubuhi na mapema siku iliyofuata kuwasaka. Kwa mujibu wa Eisner (1985), wakati katika vikatuni hutokana na msuko wa matukio katika hadithi inayosimuliwa. Sauti hii ilileta mshikamano baina ya paneli zilizotangulia kwa kubainisha wakati ambapo Malkia aliamka kwenda kuwatafuta Jipendo na Kazuri.

**Maandishi katika Mandhari ya Paneli**

Kwa mujibu wa Badman (2012), maandishi katika michoropanelini ni sehemu ya mandhari. Husomwa na wahusika kama masimulizi au hata wakayaandika. Maandishi katika mandhari ya paneli yalitoa maelezo yaliyoendeleza msuko wa hadithi. Yalikuza muwala wa hadithi kwa kudhihirisha wakati, mahali, hitimisho la hadithi na mabango ya biashara. Kwa mfano:

**Mabango ya Biashara**

Mabango ya biashara hutekeleza wajibu wake kwa kujificha katika uhalisia wake na huashiria kitu ambacho kimefichama (Fairclough, 1989), ni vigumu vijana ambao ni hadhira lengwa kuelewa athari zake. Baadhi ya kampuni zilizotangaza huduma zake katika *Shujaaz* ni zahanati za *T-safe* na *Safaricom*. Nembo za kampuni mbalimbali zilikuwa katika mabango panelini na zililenga kuwashawishi vijana kushabikia bidhaa au huduma zilizotangazwa. Ziliwabainishia vijana masuala yakuaminiwa kuhusu huduma au bidhaa. Imani iliyokuzwa huenda baadaye ikakita mizizi na kuwa itikadi (Van Dijk, 2001). Itikadi ambayo ingewaongoza kutathmini kampuni wanazopendelea huduma au bidhaa zake (Wodak, 2008). Kwa mfano:

(*Shujaaz* chapta #3, ukurasa wa 7)

Bango lenye istilahi "Safaricom" halina uhusiano na mada ya hadithi. Mandhari panelini ni mashambani kwa nyanya ya mhusika Malkia. Kwa mujibu wa Jigal (2006), aghalabu vikatuni vya Kiafrika hutangaza bidhaa katika

mazingira na wahusika mashujaa ambaoni wa Kiafrika. Ingawa, istilahi hii ilionekana kuwa na jukumu la kufahamisha kuhusu huduma za kampuni hii. Ilieneza mtazamo wa kiitikadi kama ilivyo katika diskosi za propaganda. *Safaricom* ni kampuni ya kutoa huduma za mawasiliano nchini Kenya. Uelewaji wa paneli ulichangiwa na maarifa ya kiusuli walionayo vijana kuhusu ulimwengu wanamoishi.




Nembo hii ilikuza muwala wa kijumla. Mandhari panelini ni nchini Kenya ambayo yaliipa uhalisia hadithi iliyosimuliwa. Uchanganuzi makinifu wa diskosi hutathmini michakato ya kijamii kutokana na kipindi mahususi cha kiwakati katika diskosi (Fairclough& Wodak, 1997). Nembo ya *Safaricom* iliiweka paneli hii katika kipindi maalumu cha kiwakati. Mabango ya biashara katika vikatuni hukuza muwala kwa kuashiria eneo au hurejelea suala lenye msingi ya kistoria (Kandl, 1999). Hivyo basi matukio hadithini ni baada ya kuzinduliwa kwa kampuni hii. Ina maana kuwa diskosi ya *Shujaaz* husheheni maarifa na kumbukumbu za kijamii nchini Kenya (Van Dijk, 1998). Istilahi hii ilitangaza kusambaa kwa huduma za kampuni ya*Safaricom*. Dhana ya imani iliyokuzwa ni kutokana na ukweli kuwa kampuni hii hutamalaki taratibu za kuunda fikira na mawazo ya hadhira lengwa. Mchakato huu ulifanikisha kuundwa kwa hegemoni ya soko la kutoa huduma za mawasiliano ya simu ya rununu. Hatimaye, kuhalalisha ulimwengu ambao kampuni ya *Safaricom* ilihudumu bila ya kuwa na kampuni pinzani.

**Maelezo ya Mwandishi.**

Maelezo ya mwandishi huondoa utata wa maana panelini na huelekeza msomaji katika mchakato wa ufasiri wa maana (Badman, 2012). Kwa mujibu wa Saraceni (2000), maelezo ya mwandishi aghalabu hutoa habari za kumsaidia msomaji kukarabati mtiririko baina ya paneli ili kuziba pengo lililowasilishwa kwa gata. Maelezo ya mwandishi yametumiwa kwa njia zifuatazo katika data ya utafiti huu:

**Siku ya Kutokea kwa Tukio**

Baadhi ya maelezo ya mwandishi hutaja siku maalumu ya kutokea kwa tukio. Hufafanuamandhari ya paneli. Maana ya kijumla ya paneli hujengwa kwa mandhari kuafikiana na matarajio ya hadhira kuhusu msuko wa hadithi (McCloud, 1993). Hii ni kwa sababu maana kamili ya paneli yalihalalishwa na muktadha wa mandhari. Kwa mfano:

(*Shujaaz* chapta #104, ukurasa wa 15)




Paneli zilizotangulia wahusika wamekuwa wakijiandaa kwa siku ya michuano ya urembo. Msomaji anaposoma:

*Siku ya auditions*

Siku ya michuano

Anafahamu kuwa hii ni siku ambayo wahusika walikuwa wakijiandaa kushiriki kwa kubandika mabango yaliyoihusu. Mandhari ya paneli yalifasiriwa kama ifuatayo: foleni ya watu ilitokana na idadi kubwa ya washiriki wa mashindano ya urembo. Ukumbi wa kijamii wa Jongo ulionekana ungechukua idadi kubwa ya hadhira na washiriki katika tamasha za urembo. Bango lenye picha ya mhusika wa jinsia ya kike katika ujirani wa ukumbi liliashiria kuwa washiriki ni wa jinsia ya kike pekee. Majumba yaliyorundikana kwenye ujirani wa ukumbi ni ishara kuwa huu ni mtaa wa mabanda. Huenda ndio sababu wahusika wengi walihudhuria michuano ya urembo. Hatimaye, kwa mujibu wa Saraceni (2000) msuko wa paneli hubainika kupitia upana wa paneli. Paneli ndogo huashiria muda mfupi bali paneli pana aghalabu husheheni muda mrefu usiokatizwa. Ukubwa wa paneli hii ikilinganishwa na paneli nyingine hadithini uliashiria msuko mrefu, yaani tamasha hii ilichukua muda mrefu (Saraceni, 2000). Muktadha wa mandhari uliambatana na maarifa ya kiusuli ya vijana kuhusu michuano ya mashindano ya urembo na kukuza muwala wa kijumla. Hali hii ilirahisisha uelewaji wa paneli.

**Uzungumzi Nafsi**

Uzungumzi nafsi ni usemi ambao hauhitaji majibu (Crystal & Davy, 1969). Uzungumzi nafsi ulibainika kwa maandishi au michoro kuwa ndani ya mchoro wa umbo la mawingu. Huhusisha kauli na mhusika. Aidha, huashiria fikira au mazungumzo ya mhusika (Badman, 2012). Ulikuza muwala kwa kubainisha hisia au maoni ya kibinafsi ya mhusika. Ikumbukwe kuwa uzumgumzi nafsi katika vikatuni ni kwa manufaa ya msomaji katika kukuza msuko wa hadithi. Kwa mfano:

**Uzungumzi Nafsi Unaowasilishwa kwa maandishi**

Uzungumzi nafsi uliowasilishwa kwa maandishi ulidhihirisha maoni ya mhusika kuhusu kinachotendeka panelini. Kwa mfano:

(*Shujaaz* chapta #29, ukurasa wa 3)
*Nimefika mapema hii meeting?*
Nimefika mapema kwa mkutano huu?




Nukuu hii ilidhihirisha kuwa mhusika DJ Boyie hakupata ofisi ya katibu wa kudumu ikiwa imefunguliwa. Uchanganuzi makinifu wa diskosi husaidia katika uchanganuzi kuhusu masuala yaliyofiche ambayo ni changamoto katika jamii. Istilahi "Mapema" katika nukuu hii iliashiria kuwa DJ Boyie alifika kabla ya ofisi ya katibu wa kudumu kufunguliwa. Licha ya kuwa wakati rasmi wa ofisi za kiserikali kufunguliwa. Iliangazia changamoto zilizowakumba vijana waliotafuta huduma za serikali. Kauli ya mhusika Boyie panelini ilikuza muwala kwa kuweka wazi mtazamo wa mwandishi kuhusu kuchelewa kufunguliwa kwa ofisi za serikali. Kwa mujibu wa Blommaert (2005), uchanganuzi makinifu wa diskosi ni kuchunguza athari za mamlaka katika diskosi iliyozalishwa katika matumizi ya jumla ya muktadha wa matumizi ya diskosi. Huenda mhusika DJ Boyie hakusema kwa sauti kwa kuhofia kuwa mhusika mwenzake aliye na mamlaka kumpiku angemsikia na huenda hangemhudumia.

**HITIMISHO**

Lengo la makala hii lilikuwa kueleza namna muwala ulivyopatikana katika vikatuni vya *Shujaaz*. Nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi ilikuwa dira katika uchanganuzi wa data. Kulingana na data ya makala hii muwala katika *Shujaaz* ulitokea katika viwango vitatu: namna paneli zinavyohusiana kimaana ili kukuza msuko wa matukio katika diskosi ili kujenga diskosi nzima, namna diskosi inavyohusiana na maarifa ya kiusuli yanayojenga muwala wa kijumla na muwala uliokuzwa na mada. Muwala wa kijumla ulikuwa mpana na ulihitaji muundo mkubwa ilhali muwala uliotokana na msuko wa matukio haukuwa umebainika barabara na haukuhitaji muundo mpana. Muwala katika sampuli ya jarida hili ulikuzwa na: mada, sauti za kionomatopeya, maandishi katika mandhari ya paneli, maelezo ya mwandishi na uzungumzi nafsi.

## MAREJELEO


Badman, D. A. (2012). *Panel & Pictures: Text in Comics, ComixTALK*, http://comixtalk.com/panels_pictures_text_comics, retrieved on 1st March, 2020.

Beck, M. R. (1999). *Comics in Swahili or Swahili Comic*? AAP 60 (1999) 67-101.

Bhatia, A. (2013). Critical Discourse Analysis: History and New Development: In C.A Chepelle (ed) *The Encyclopedia of Applied Linguistics*, Oxford, UK: Wiley-Blackwell.

Brown, G., & Yule, G. (1983). *Discourse Analysis*, Cambridge: Cambridge University Press.

Coulthard, M. (1981). *An Introduction to Discourse Analysis* (2nd edition) London: Longman.

Crystal, D., & Davy, D. (1969). *Investigation English Style*. London: Longman Group.

Danes, F. (1974). Functional Sentense Perspective and the Organization of Text, In Danes F. (Eds), *Paper in Functional Sentense Perspective*, Prague: Academia, 106-128.

Dofs, E. (2008). *Onomatopoeai and Iconicity. A Comparative Study of English and Swedish Animal*, Karlstads University Press: Karlstads, Sweden.

Eisner, W. (1985). *Comics and Sequestial Art*, Tamarac, FIorida: Poorhouse Press, USA.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*, New York: Longman, US.

Fairclough, N. (1992). Discourse and Text. Linguistic Intertextual Analysis within Discourse analysis, in: *Discourse and society*, SAGE Publication Limited, California: USA, 3:193-217.

Fairclough, N. (1995). *Critical Discourse Analysis: The Critical Study of Language*, London: Longman.

Fairclough, N. & Wodak, R. (1997). Critical Discourse Analysis. In Ed. Van Djik, T. *Discourse Studies*: A *Multidiscplinary Introduction*. pp 258-284. London: Sage.

Gay, M. (1992). *Educational Research: Competence for Analysis and Application (3rd edition)*, Meril Publishing Company, Idianopolis, Indiana: USA.

Groensteen, T. (1999). *Systeme de la Bande Dessinee,* Frace: Presses Universitaires de Frace.

Groensteen, T. (2007). *The System of Comics*, Mississip: University of Mississipi.

Habwe, H. J. (1999). Discourse Analysis of Swahili Political Speeches, (PhD thesis, Unpublished), University of Nairobi, Nairobi, KENYA, http://erepository.uonbi.ac.ke:8080/xmlui/handle/123456789/1 7941.retrieved on 11/02/2018.

Harvey, R. (2001). Comedy at Juncture of Word and Image, in: *The Language of Comics: Word and Image*, Jackson: University Press Mississipi.

Jacobs, D. (2007). More than Words: Comics as a Means of Teaching Multiple Literacies, *The English Journal*, 96(3), 19-25.

Jigal, B. (2006). Stupid Hares and Margarine: Early Swahili Comics in: L. John, *Cartooning in Africa*, Cresskill: Hampton Press.

Kale, J. 2003. *Language as Social Practice*, PASTEP, Australian Agency for International Development.

Kothari, C.R. (2009). *Qualitative Technique*, 3E. Vikas Publishing House PVT LTD.

McCloud, S. (1993). *Understanding Comics: The Invisible Art*, Northampton MA: Kitchen Sink Press.

Mugenda, O. M., &Mugenda, G. A. (1999. *Research Methods: Quantitativeand Qualitative Approaches.* Nairobi; Acts Press.

Mulusa, T. (1990). *Evaluation Education and Community Development Programmes*, Nairobi Universiry Press, Nairobi: Kenya.

Nangira, E. E. (2004). Usomekaji katika Fasihi Tafsiri: Uchambuzi wa Matini Madhabahu ya Kilio, (Tasnifu ya Uzamili haijachapishwa), http://erepository. uonbi.ac.ke.8080/xmlui/handle/123456789/53210 retrieved on 08/07/2020.

Neil, C. (2005). Un-Defining Comics: Separating the Cultural from the Structural in Comics. *International Journal of Comic Art*,7 (2).

Neil, C. (2012). Comics, Linguistics and Visual Language: The Past and Future of a Field in: F. Bramlett (Ed) *Linguistics of the Study of Comics*, New York: Palgrave Mcmillan.

Petersen, R. S. (2007). The Acoustic of Manga: Narrative Erotics and Visual / Presence of Sound, *International Journal of Comics Art*, 9(1): 578-590.

Saraceni, M. (2000). *Language beyond Language: Comics as Verbo-Visual Text*, University of Nottingham.

Taylor, S. (2001). Locating and Conducting Discourse Analytic Research. In M. Wetherell, S. Taylor na S. J. Yates (Eds). *Discourse as a Data: A Guide for Analysis* (p. 5-48), Sage Publication, London.

Van Dijk, T. A. (1987). *Discourse and the Reproduction of Racism,* University of Amsterdam. Centre for Race and Ethnic Studies.

Van Dijk, T. A. (1998). *Ideology: A Multidisciplinary Approach*, Sage Publications, California: USA.

Van Dijk, T. A. (2001). Critical Discourse Analysis, in D. Schiffrin, D. Tannen and H.E. Hamilton (eds) *Handbookof Discourse Analysis*. Oxford: Blackwell.

Van Dijk, T. A. (2002). Media Context: The Interdisciplinary Study of News as Discourse, in: *A Hand Book ofQualitative Methodologies for Mass Communication Research*, Routledge, p.122-134.

Wang, Y. & Guo, M. (2014). A Short Analysis of Discourse Coherence in: *Journal of Language Teaching andResearch*, 5(2) 460-465. Retrieved Match 16th 2020 from http://dx.doi.org/10.430/jltr.5.2.460-465.

Wodak, R. (2008). Introduction: Discourse Studies-Important Concept and Terms, In: R, Wodak & M.Krzyzanovosk (eds.). *Qualitive Discourse Analysis in Social Science. Palgrave Basingstoke*, p. 1-29.